**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

Tovuti:www.butimbatc.ac.tz
Baruapepe:butimbatc@moe.go.tz
Simu:+255768266944

**Unapojibu tafadhali rejea:**
**Kumb.Na.BCE/ET/37/94/**

Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Ualimu Butimba,
S.L.P. 1411,
**MWANZA**

**30 MAY, 2025**

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHADA YA UALIMU ELIMU MSINGI (MIAKA MIWILI) AUGUST, 2025**

## 1.0: UTANGULIZI: -

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya **STASHAHADA YA UALIMU ELIMU MSINGI MCHEPUO WA SANAA NA MICHEZO (kwa lugha ya kiingereza)** katika chuo cha Ualimu Butimba mwaka wa masomo **2025/2026**. Chuo kinakupongeza kwa kupata nafasi hii. Tunategemea kuwa utaitumia nafasi hii vizuri katika masomo yako. Unaelekezwa kuweka juhudi na kuwa na moyo wa kujifunza darasani na nje ya darasa ili uweze kufaulu vizuri mafunzo yako.

## 2.0: MAHALI CHUO KILIPO: -

Chuo kipo mkoa wa Mwanza katika Halmashauri ya jiji la Mwanza kilomita nane (08) kutoka mjini kati. Kuna njia kuu tatu za kukuwezesha kufika chuoni. Iwapo unatokea mjini kati panda daladala zilizoandikwa BUTIMBA TTC ambazo zitakufikisha hadi lango kuu la kuingia chuoni. Iwapo unatokea stendi kuu ya mabasi Nyegezi panda daladala zinazoelekea mjini na shukia Mkuyuni sokoni (Butimba Kona) au iwapo utatokea stendi kuu ya mabasi Nyamongolo panda gari zinazoenda Nyashishi /Usagara pia shukia Mkuyuni Sokoni (Butimba Kona) na hapo utapata usafiri mwingine wa daladala zitokazo mjini Mwanza kwenda chuoni Butimba. Pia upo usafiri wa taxi kutoka hapo Butimba kona. Tusingeshauri sana usafiri wa bodaboda ambao pia unapatikana.

## 3.0: TAREHE YA KURIPOTI CHUONI

Wanachuo waliochaguliwa kujiunga na mafunzo ya **stashahada ya ualimu elimu msingi** wanatakiwa kuripoti Chuoni tarehe **18/08/2025** ili kuanza mafunzo na mwisho wa kuripoti ni tarehe **30/08/2025**. Baada ya tarehe hiyo, mwanachuo aliyechelewa atapoteza sifa za kujiunga na Chuo.

Mwanachuo afikapo Chuoni, anaekezwa kuripoti kwa Msajili wa wanachuo ili aweze kusajiliwa. Mwanachuo huruhusiwi kwenda Bwenini au maeneo mengine ya chuo kabla ya kupewa utaratibu toka Ofisi ya Usajili.

**4.0: MUDA WA MAFUNZO: -**

Muda wa mafunzo kwa wanachuo wa **stashahada ya ualimu elimu msingi** kwa sifa za **kidato cha sita**, na wahitimu wa ngazi ya cheti ni miaka miwili (**2025 - 2027**).

**5.0: MAHITAJI YAKO BINAFSI MWANACHUO NA YA TAALUMA: -**

- Shuka jozi 2 za rangi ya bluu bahari (light Blue) na mto wenye foronya ya bluu Bahari.
- Ndoo.
- Chandarua cha mbu.
- Daftari 8 (Counterbook quire two)
- Bukta ya bluu, fulana nyeupe na tracksuit ya blue.
- Raba nyeupe za michezo.
- Sahani, bakuli, kikombe na kijiko.
- Hati ya uthibitisho wa Daktari (imeambatanishwa).
- Sketch book
- Hb pencil set
- Acrylic water colour (1set)
- Artistic brush (1 set)

**6.0: VYETI HALISI:**

- Fika na **CHETI HALISI (Original Academic Certificate)** cha Kidato cha NNE (**na kopi zake 02) na kidato cha SITA /GRADE A (na copy mbili)**. Wahitimu wa kidato cha sita/cheti (GTCE) kwa mwaka **2025** waje na **result slip (na kopi zake 02)** wakati wakisubiri vyeti halisi kutoka, na mara tu vitakapotoka utatakiwa kuleta cheti halisi cha ngazi husika.
- Fika pia na cheti cha kuhitimu kidato cha NNE (**Leaving Certificate na kopi zake 02),** isipokuwa kwa wahitimu wa kujitegemea **(Private Candidates).**
- Fika na cheti halisi cha kuzaliwa (**na kopi zake 02)**

*Muhimu:*

**Mwanachuo ambaye hatakuja na vyeti tajwa hapo juu, hatapokelewa chuoni.**

**ANGALIZO:** Ikiwa wewe ni Mtumishi (Mwajiriwa) njoo na kitambulisho chako halisi cha kazi na barua ya ruhusa kutoka kwa mwajiri wako.

**7.0: ADA YA CHUO:**

**Ada** ya Chuo ni Tshs. **450,000/=** kwa mwaka. Ada hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili yaani Tshs. **225, 000/=** kwa muhula au unaweza kulipa kiasi chote Tshs. **450,000/=** kwa mara moja kwa mwaka.

Ada ya Chuo ilipwe kwa namba ya kumbukumbu (**control number**) inayotolewa na ofisi ya uhasibu na usajili. Mawasiliano na ofisi kupata namba ya kumbukumbu yafanyike kwa namba: **0626 204 966 (Mhasibu)** Au **0755 646138 (Msajili)** au **0653144 677 (Msajili)** Namna ya kupata namba ya kumbukumbu(control namba) ;tuma ujumbe mfupi(sms)kwenye namba za simu tajwa hapo juu ukionyesha majina yako kamili,mwaka unaosoma na kiasi cha malipo unachotaka kufanya(mfano JUMA HAMISI CHERAHANI, **stashahada ya ualimu elimu msingi mwaka wa kwanza miaka miwili kiasi ninacholipa 450,000)**

## 8.0 MICHANGO MINGINE

Michango mingine ya chuo ni **Tshs 150,000/=**. Fedha ya michango ilipwe kwenye akaunti ya chuo **Na: 31101200023 Benki ya NMB.** Jina la akaunti ni ***Butimba Teachers Training College.***

**MUHIMU SANA:**

I. T-shirts yenye nembo ya chuo itapatikana chuoni kwa kiasi cha shilingi **15,000.00** tu ilipwe kwenye akaunti ya michango **Na: 31101200023 Benki ya NMB**. Jina la akaunti ni **Butimba Teachers Training College**.

II. Mwanachuo aje na ***'Bank* Pay in Slip' au** Stakabadhi inayotolewa na Benki husika. Unatakiwa uje na *Stakabadhi/Pay in Slip* mbili, moja inayoonyesha malipo ya ada ya chuo na nyingine ionyeshe michango mingine ya chuo.

III. Fanya malipo sahihi kwenye akaunti sahihi kuepuka usumbufu.

IV. Stakabadhi za malipo zionyeshe jina kamili la mwanachuo na si jina la mzazi/mlezi anayefanya malipo.

V. Wakati wa kulipa yaandikwe majina sahihi ya mwanachuo yote matatu/mawili kulingana na yanavyotumika kwenye vyeti vyako halisi vya kidato cha NNE/SITA/GATCE.

## 9.0: VIFAA VINGINE KWA AJILI YA MATUMIZI YA CHUO:

Kila mwanachuo anaelekezwa kuja na vifaa vifuatavyo:

i. Bunda (01) la karatasi (**DOUBLE A**).
ii. Flat file (01)
iii. Bahasha (01) ya A4 kwa ajili ya kutunzia vyeti.
iv. Nakala (02) za vyeti.
v. Nakala (02) za kila stakabadhi ya malipo utakayofanya.

**10: SARE YA CHUO: -**

**A. Wanawake:**

- Sketi nyeusi mbili (02) zenye kuvuka magoti cm 3 zikiwa na rinda moja tu (Tazama mchoro Na. 1 hapo chini).
- Shati mbili (0 2) zenye rangi ya buluu bahari (light blue) mikono mirefu.



- Koti la suti rangi nyeusi.
- Tai nyeusi ndefu mbili (0 2).
- Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi jozi mbili (02).
- Soksi nyeupe jozi mbili (02).

**Angalizo:** Kwa wanachuo wanaovaa hijab, suruali mbili nyeusi pana, blauzi ndefu kuvuka magoti na kitambaa cha kichwani rangi ya buluu bahari (light blue). Kanga na mitandio siyo sehemu ya hijab kwa mujibu wa sare za chuo.


**B. Wanaume:**

- Suruali nyeusi mbili (02) zenye marinda (Tazama mchoro Na.2 hapo chini).
- Shati mikono mirefu mbil i (02) rangi ya bluu bahari




- Tai mbili nyeusi (02).
- Viatu vyeusi j oz i mbili (0 2).
- Soksi nyeusi jozi mbili (02).
- Koti la suit   rangi nyeusi.

Mchoro Na. 1



Mchoro Na. 2



**11.0: USAFIRI: -**

Nauli ya kuja chuoni na kurudi nyumbani itagharimiwa na mwanachuo husika.

**12.0: CHAKULA: -**

12.1: Chakula kinapatikana chuoni;aidha mwanachuo hataruhusiwa kujipikia mwenyewe.hivyo USIJE NA SUFURIA AU JIKO LA KUPIKIA.

12.2: Chuo hakina chakula maalum **(special diet)** kwa wanachuo wenye changamoto za kiafya.

**13.0: MAWASILIANO:**

Mawasiliano yoyote yanayokuhusu wewe kutoka kwa ndugu zako au nyumbani LAZIMA yapitie kwenye uongozi wa Chuo, kwa Namba: **0784 563 045** (Makamu Mkuu wa Chuo), **0755 646 138** (Msajili wa Wanachuo) na **0783 413 546** (Mratibu wa masuala ya wanachuo).

14.0: **NIDHAMU**

Wakati wote uwapo hapa Chuoni unatakiwa kufanya mambo sahihi kwa wakati sahihi, kuwa mahali sahihi, na kupita njia sahihi kwa mujibu wa KANUNI**/SHERIA** za chuo ambazo utazipata mara ufikapo Chuoni.

15: **MWISHO: -**

Tunategemea kuwa utakuwa mfano mzuri wa kuigwa na wanachuo wenzako, walezi na jamii kwa kutekeleza **"MOTTO"** wa Chuo **"JUHUDI NA MAARIFA".**

**KARIBU CHUO CHA UALIMU BUTIMBA**

NICHOLAS A MAGIGE

MKUU WA CHUO

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU BUTIMBA
S. L. P. 1411 MWANZA

**Nakala**: Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo cha Ualimu Butimba

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**

Website: www.butimbatc.ac.tz
Email:butimbatc@moe.go.tz
Phone No.: +255768266944
In reply please refer:

Principal,
Butimba Teachers College,
P.O.Box 1411,
**MWANZA**

**Ref.No.BCE/ET/37/94/87**

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

**PART A:**

To the Medical Officer;

……………………………………………..

Please examine *Mr/Mrs/Miss ……………………………………… (Name in Full) as to his/her physical and mental fitness for enrolment as a student teacher.

The examination should include but not limited to the following categories:

1. (a) Eye sight
   (b) Hearing
   (c) Speech
   (d) Venereal Diseases
   (e) Leprosy
   (f) Limbs
   (g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other medical condition.
4. Blood Group
5. Pregnancy (if applicable)

Date: …………………………. Signature……………………

**PARTB:** **MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by Government Medical Officer)

1. (a) Eye sight ……………………………………………………………………
   (b) Hearing …………………………………………………………………....
   (c) Speech ……………………………………………………………. …
   (d) Venereal Diseases ……………………………………………………………
   (e) Leprosy …………………………………………………………………….
   (f) Limbs ……………………………………………………………………………….
   (g) Epilepsy ……………………………………………………………………………
2. Neuroses…………………………………………………………………………………
3. Other medical condition……………………………………………………………….
4. Blood Group ……………………………………………
5. Pregnancy (if applicable) …………………………………………………………….

   I have examined the above-named student that he/she is physically fit/unfit and mentally*fit/unfit for enrolment as a student teacher.

Date: ----------------------------      Signature & Stamp……………………………………………

Station …………………………………………   Designation ………………………...…..….



**SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA MWENENDO BORA WA MWANACHUO**

Tabia na mwenendo wa mwalimu ni mfano wa kuigwa kwa wanafunzi wake na jumuiya inayomzunguka. Maneno na matendo yake yawe mifano mizuri inayofaa kuigwa. Kwa kuwa ualimu bora huanzia chuoni, kazi kubwa ya Chuo cha Ualimu ni kuandaa walimu bora wenye haiba ya ualimu ili kuwafanya waishi kwa usalama, amani, matumaini, heshima na mafanikio. Hivyo, kila Chuo hakina budi kuwa na kanuni bora kama ilivyofafanuliwa:

a) **Afya**
   i. Kabla ya kusajiliwa, kila mwanachuo lazima apimwe afya na awe na cheti cha daktari wa Serikali kinachoonesha kwamba afya yake ni nzuri kwa ajili ya kupata afua stahiki wakati wa mafunzo ya ualimu;
   ii. Mwanachuo mwenye ujauzito atalazimika kuahirisha mafunzo ya ualimu;
   iii. Mwanachuo aliyetoa mimba au atakaye jaribu kutoa mimba ataachishwa mafunzo ya ualimu;
   iv. Mwanachuo haruhusiwi kutumia vilevi au madawa ya kulevya

b) **Mavazi**
   i. Mwanachuo anapaswa kuvaa sare safi, zisizobana na nadhifu wakati wote wa vipindi na akiwa nje ya Chuo; na
   ii. Mwanachuo anapaswa kuwa na sare maalumu za michezo na zivaliwe wakati wa michezo.

c) **Heshima na Utii**
   i. Mwanachuo anapaswa kujiheshimu na kuwa na lugha yenye hadhi ya ualimu na matendo yake yawe yanakuza heshima yake;
   ii. Mwanachuo awaheshimu wenzake, wafanyakazi wa Chuo na jamii inayomzunguka;
   iii. Mwanachuo haruhusiwi kwenda nyumbani kwa mkufunzi au mfanyakazi mwingine pasipo ruhusa maalumu;
   iv. Mwanachuo wa kike haruhusiwi kwenda kwenye bweni la wavulana au mvulana kwenda kwenye bweni la wasichana isipokuwa kwa kibali maalumu cha Mratibu wa Masuala ya Wanachuo;
   v. Wanachuo wa kike na wa kiume hawapaswi kuonesha kwa njia yoyote ile kwamba wanaishi kama mtu na mpenzi wake;
   vi. Mwanachuo haruhusiwi kuwa na tabia ya uasherati, usagaji, ushoga, ubakaji, unajisi au uzinzi na mtu yeyote yule;
   vii. Mwanachuo sharti afike kwa wakati anapoitwa kwa kengele au ishara zingine mahali popote anapohitajika kama vile ukumbini, darasani, katika kazi za nje n.k
   viii. Mwanachuo haruhusiwi kutoa au kusambaza taarifa za uongo, kufitini, kuzusha mambo yanayoweza kuleta taharuki na kuvunja amani ya Chuo.

d) **Usafi**
   i. Mwanachuo anapaswa kuzingatia usafi wa mwili, ikiwa ni pamoja na kuwa na nywele fupi, kukata kucha na kunyoa ndevu;
   ii. Mwanachuo anatakiwa kuweka sehemu yake ya malazi katika hali ya usafi muda wote;
   iii. Mwanachuo anapaswa kushiriki kikamilifu katika shughuli za usafi katika mazingira ya Chuo.

**e) Kazi**

i. Mwanachuo anapaswa kufanya kazi anazopewa kwa ufanisi na kwa wakati; na
ii. Mwanachuo anapaswa kuheshimu na kufanya kazi za mikono kwa weledi.

**f) Masomo**

i. Mwanachuo anapaswa kuhudhuria vipindi vyote vya masomo na vya kujisomea kwa mujibu wa ratiba ya Chuo;
ii. Mwanachuo anapaswa kuhudhuria na kufanya mazoezi, majaribio na mitihani yote inayotolewa;
iii. Mwanachuo anapaswa kufaulu mazoezi, majaribio na mitihani itakayofanya kulingana na kiwango kilichowekwa;
iv. Mwanachuo anapaswa kujiandaa vizuri na kufanya mazoezi ya kufundisha kwa muda na kwa utaratibu uliopangwa; na
v. Mwanachuo anapaswa kuhudhuria darasani siku zote za masomo kulingana na muhula husika.

g) Mali na vifaa

i. Mwanachuo haruhusiwi kuiba, kuharibu, kupoteza mali ya umma au ya watu wengine;
ii. Mwanachuo ana wajibu wa kulinda na kutunza mali yake binafsi, za wanachuo wenzake na mali ya umma;
iii. Mwanachuo anapaswa kujiepusha na vitendo vya ubadhirifu na ufujaji wa mali ya umma kama vile maji na umeme;
iv. Mwanachuo anapaswa kutunza na kurejesha kwa wakati vifaa anavyoazima au kukabidhiwa kama vile vitabu, vifaa vya darasani, bwaloni na bwenini; na
v. Mwanachuo anapaswa kuzingatia matumizi sahihi ya vifaa vya mawasiliano kwa kufuata sheria na taratibu za Chuo na nchi.

**h) Ruhusa**

i. Mwanachuo anapaswa kuomba ruhusa kila anapotoka nje ya Chuo;
ii. Kutakuwa na muda maalumu wa kuitisha majina ambao kila mwanachuo lazima ahudhurie kwa utaratibu utakaopangwa na Chuo;
iii. Mwanachuo haruhusiwi kutembelea kumbi za starehe, nyumba za wageni na vilabu vya pombe; na
iv. Mwanachuo haruhusiwi kumkaribisha mgeni katika mazingira ya Chuo bila kibali.

**i) Sheria za Nchi**

i. Mwanachuo anapaswa kufuata maagizo na Sheria za nchi;
ii. Mwanachuo anapaswa kuwa na heshima kwa viongozi wa Chuo na Serikali;
iii. Mwanachuo anapaswa kuheshimu alama za Taifa, ikiwa ni pamoja na Bendera, Wimbo na Nembo ya Taifa (Ngao ya Taifa);
iv. Ni kosa kwa mwanachuo kutumia nafasi au uwezo wake kushawishi wenzake ama watu wengine wasitii Serikali halali ya nchi au chombo chochote halali cha Serikali; na
v. Mwanachuo anapaswa kuzifahamu na kufuata Kanuni, Taratibu na mwenendo mwema wa maadili ya ualimu.